**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Arusha Girls High School,
S.L.P. 16034,
EMAIL :arushagirlz@gmail.com **ARUSHA**

24/4/2024

Namba za simu.

**Mkuu wa shule: 0784258018 / 0769121516**

**Makamu mkuu wa shule: 0784137840 / 0755 845604**

MZAZI WA ____________________________________

S.L.P. ________MKOA___________________________

PICHA P/S YA WAZAZI NA MTOTO

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ARUSHAGIRLS' HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA MKOA WA ARUSHA MWAKA 2024 KIDATO CHA TANO.**

1.0 . Nafurahi kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano(V) katika shule hii mwaka 2024 kwa tahasusi ya

| HGE | EGM | PGM | PCM |
|---|---|---|---|

Shule ya Sekondari Arusha Girls ipo umbali wa kilometa 09 (tisa) Magharibi mwa mji wa Arusha.Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana katika kituo cha mabasi Kilombero magari ya kwenda Kisongo nauli ni shilingi 700/= hadi njia panda ya kwenda shuleni panajulikana kwa jina ndorobo.Unaweza kuchukua usafiri wa pikipiki hadi shuleni. Gharama yake ni shilingi shilingi 2000/=. Zingatia Tangazo la TAMISEMI kuhusu tarehe ya kuripoti Shuleni.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE YA SHULE.**

a) Sare ya shule ni

1 Sketi rangi ya orange karoti mbili (02) , urefu juu kidogo ya unyayo na isiyobana mwili. Hatupokei kabisa sketi fupi. Angalia kielelezo cha picha hapo chini.

2. Mashati meupe mikono mifupi mawili (02)

3. Tai ya rangi ya orange karoti mbili (02)

4. Sweta nyeusi moja (01) unaweza lipata Jirani na shuleni

5. Soksi nyeupe jozi mbili (02) (Stockings)
6. T-shirt nyeupe moja (01) unaweza lipata Jirani na shuleni
7. Nguo ya kushindia (Shamba dress) rangi ya kahawia na nyeupe (draft) mtindo wa soro.
8 Hijab (kijuba) nyeupe inayoishia chini ya kifua (kwa waislamu)
9 Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.
10. Sare ya michezo ni Bukta moja rangi ya blue,Sketi fupi (nap round) ya blue,T-shirt nyeupe,Raba nyeupe na Soksi nyeupe.
11. Track suit rangi ya light bluu
12. Poolneck nyeupe na jackect nyeusi lisilo na maandishi kwa matumizi ya. wakati wa baridi na mvua.



*Kielelezo cha mfano wa sare ya shule*

**ZINGATIA**: Katika kukamilisha sare ya shule, nywele lazima ziwe fupi za kuchana, kucha ziwe fupi na zisipakwe rangi na uvaaji wa mapambo yoyote HAUTAKIWI.

**2.2 MICHANGO YA SHULE.**

**MICHANGO ANAYOTAKIWA KULIPA MZAZI.**

i. Nembo shilingi 5,000/=
ii Kitambulisho cha shule Shilingi 5,000/=

iii. Tahadhari shilingi 5,000/=

iv. Uendeshaji wa shule Shilingi 65,000/=

**Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunt ya shule namba. 42710006675 Benki ya NMB Jina la Account ni Arusha Girls High School. (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye "pay in slip").**

**c) MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI:-**

i **Rimu moja aina ya double A (a 1 ne ) Photocopy paper size A4.**

ii. **Folder File ya kaki moja**, tafadhali usilete box file.

iv. Scientific calculator.

v. Madaftari ya kutosha ya masomo yake, Mathematical set, Graf pad, Kalamu na vifaa vingine vya kujifunzia.

vi. Begi la mgongoni la kuhifadhia vifaa vya darasani.

vii. Sahani ya mfupa moja, kikombe kimoja rangi ya maziwa na kijiko kimoja..

viii. Rato (01) kwa mchepuo wa PGM ,Jembe (01) kwa mchepuo wa EGM, Fyekeo (01) kwa mchepuo wa PCM, Fagio ya chelewa (01) kwa mchepuo wa HGE.

## 3.0 MAHITAJI YA MALAZI YA BWENI.

i. Chandarua ya rangi nyeupe (01)

Ii Shuka rangi ya pink nne (4).na foronya za pinki (2).

iii. Blanketi moja (1) na mto wa kulalia.

iv. Nguo za kulalia.

V. Sanduku imara la kuhifadhia mali yako. **Tunapokea sanduku moja tu aina ya tranka.**

vi Fedha ya kukodi godoro shilingi elfu kumi kwa mwaka,iletwe shuleni.

Vii Taulo moja na vitenge doti moja.

viii. Mahitaji yote ya bafu kwa mfano. sabuni, mafuta, dawa ya meno.

ix Ndoo moja ya kuogea na chupa ya kuhifadhia maji safi ya kunywa.

xi. Tochi 1 ya solar

x. Gum- boots kwa matumizi ya kazi za nje ya darasa na kipindi cha mvua.

**MHIMU** :Hakikisha unatimiza mahitaji yote kuepuka usumbufu usio wa lazima kwani shule ipo nje ya mji

**4.0 MUHIMU KWA WANAJUMUIYA YA ARUSHA GIRLS HIGH SCHOOL.**

4.1 Wanafunzi wote lazima wafuate sheria za NCHI na za shule kwa ujumla.

Lengo la sheria za shule yetu ni kumjenga mwanafunzi kuwa na mwenendo mzuri kitabia hivyo kumwezesha kufanikiwa kupata kile anachostahili haswa **Taaluma.**

Sheria hizi zitasaidia kuleta hali ya AMANI, UMOJA na FURAHA shuleni na kumfanya kuwa raia mwema . Kila mwanafunzi aje na nia ya KUSOMA KWA BIDII, KUJITUMA na ajitahidi kuishi vizuri katika jumuiya ya shule hii na majirani zetu pia

**4.2** Kwa upande wa shule sisi WALIMU pamoja na WAFANYAKAZI WASIO WALIMU tutajitahidi kumfundisha na kumlea mtoto katika maadili mema lakini tutashindwa kazi hii endapo hatutapata ushirikiano mzuri wa wazazi/walezi.Tunaomba ushirikiano wenu

Kila mtu anatakiwa Kuheshimu:

- **i.** **Bendera ya Taifa** na **picha za viongozi wa serikali**
- **ii.** **Nembo ya Taifa "coat ofArms", wimbo wa Taifa na fedha za Taifa**

Lugha inayotumika darasani na nje ya darasa ni Kiingereza tu. Hii inasaidia kuleta ufanisi katika masomo. Kwa vile shule ni mahali pa kusoma **kelele hazitakiwi kabisa** madarasani na sehemu nyingine za kujifunzia.

**4.3** Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyompasa kama Ratiba ya Shule inavyooelekeza. Kazi za mikono ni sehemu ya elimu inayotolewa hapa shuleni. Kila mmoja lazima ashiriki kikamilifu kazi za mikono.

## 5.0 SHERIA ZA SHULE

i **Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini na darasani.**

ii. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa za aina yoyote. Mwanafunzi anapolazimika kuwa na dawa atoe taarifa kwa matroni ili aweze kuhifadhiwa. Wanafunzi hawaruhusiwi kupeana dawa shuleni.

iii Wanafunzi hawaruhusiwi kuongea na mgeni yeyote bila ruhusa ya Mkuu wa Shule/makamu mkuu wa shule/mwalimu wa zamu

iv Kupata, kutoa mimba ni mambo ambayo shule hii haitegemei kwa vile kila msichana Mwema anamcha Mungu na ana malengo mazuri katika maisha yake.

v .Kila mmoja anawajibika kuvitunza kwa uangalifu wa hali ya juu vifaa vyote vya shule atakavyokabidhiwa na asivyokabidhiwa.Uharibifu wowote utakaotokea gharama za matengenezo zitalipwa na atakayehusika na uharibifu huo. Mfano, Kuvunja vioo vya madirisha, milango madawati, viti .

vi. Wakati wa kutoka na kuingia shuleni lazima mwanafunzi awe katika sare kamili.

vii. **Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda kwenye nyumba zawalimu/wafanyakazi bila kibali** cha Mkuu wa Shule.

**N.B** Kila mwanafunzi anategemewa kuwa na heshima kwa watu wote hapa shuleni na kwa wageni , pia atumie lugha nzuri wakati wote na aeleze matatizo yake kwa viongozi wanaohusika, awatii viongozi wote na ashirikiane na wenzake kwa upendo, heshima, amani na udugu.

## 6.0 MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo wowote ule.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati,uhusiano wa jinsia moja na kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. **Kumiliki / kutumia simu ya mkononi na aina yoyote ya vifaa vya kielectroniki katika mazingira ya shule** bila kibali cha Mkuu wa Shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvi. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
xvii. Kulala nje ya shule bila ruhusa
xviii. Kutoka nje ya mipaka ya Shule bila kibali kutoka kwa Mkuu wa Shule.

## 7.0 VIAMBATANISHO MUHIMU.

a) Fomu ya utii na tabia njema kwa mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo,fujo,makosa ya jinai n.k

b) Fomu ya mzazi/mlezi historia na kukiri kukubaliana na sheria,kanuni za shule

na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

c) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination form).ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali.**Tafadhali ambatanisha majibu ya vipimo** .

d) Passport size ya Mwanafunzi, Baba ,Mama au Walezi wake.

**ZINGATIA :Tafadhali jaza fomu zote kwa ukamilifu**

**FOMU YA UTII NA TABIA NJEMA**

Mimi ------------------------------------------------------------------ (jina kamili la mwanafunzi)

Kidato cha -------------------------- mwaka ------------------

Natambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi na naahidi kwamba:-

a) Nitatii na kuwaheshimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya darasa, viranja, walimu, watumishi wote hadi Mkuu wa Shule.
b) Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
c) Sitashiriki katika mgomo,Fujo na makosa ya jinai.
d) Sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali maalumu kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.
e) Kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali ichukuliwe dhidi yangu ni pamoja na kusimamishwa masomo ama kufukuzwa shule.

Tarehe _______________ Jina na Sahihi ya Mwanafunzi________________________________

Tarehe___________Jina la Mzazi/Mlezi_______________________________________________

Sahihi ya Mkuu wa Shule____________________________

**FOMU YA TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Baba -----------------------------------------------------------------------
   Kabila lako ni …………………………………………………………………..
   Kazi yako-----------------------------------------------------------------------------------
   Anwani ya mahali pa kazi ya baba -------------------------------------------------------
   Nambari ya simu -------------------------------------------------------------------------
2. Jina kamili la Mama ------------------------------------------------------------------
   Kabila lako ni …………………………………………………………………..
   Kazi yake ----------------------------------------------------------------------------------
   Anwani ya mahali pa kazi ya mama ------------------------------------------------------
   Nambari ya simu -------------------------------------------------------------------------

3. Jina kamili la Mlezi (iwapo mtoto ni yatima)

   -----------------------------------------------------------------------------------------------

   Kazi na Anwani yaMzazi/ Mlezi ---------------------------------------------------------

   -----------------------------------------------------------------------------------------------
4. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto) au ‘Place of Domicile’

   Kijiji/Mtaa ------------------------------------ Wilaya ---------------------------------------

   Kata --------------------------------------------- Mkoa -----------------------------------------

   Tarafa -------------------------------------------
5. Mtoto a na (i) Baba tu (ii) Mama tu (iii) Wazazi wote
6. Dini ya Baba ------------------------------------------- Dhehebu --------------------------

   Dini ya Mama --------------------------------------- Dhehebu --------------------------

   Dhehebu unalotaka mwanao alelewe -----------------------------------------------------
7. Mahali na namba ya mlezi anayeishi Arusha ambaye tutashirikiana kwenye matatizo ya kiafya ya mwanafunzi ---------------------------------------------------------------------

Mimi ------------------------------------- (Baba/Mama/Mlezi) wa ------------------------------

Nimesoma na kuelewa sheria na kanuni za shule.Nakubali kulipa Ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

Tarehe ---------------------------------------------

Jina la Mzazi/Mlezi…………………………… ……………….

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………

**MHIMU SANA**: Hakikisha umemkatia bima ya afya mwanao. Kwa wale ambao hawatakuwa na bima ya afya hukatwa shuleni kwa vikundi vya wanafunzi miamoja kwa shilingi 50,400/= kupitia Mfuko wa bima ya afya. Hivyo usiweke fedha kwenye akaunti ya shule.

## 6.0 **VITABU**

Ifuatayo ni baadhi ya orodha ya vitabu vinavyotumika darasani.

**ECONOMICS:**

1. Text Book of Economics by J.L. HANSON
2. Economic Simplified by SALEEMI
3. Modern economic’ by KHAN.
4. Macro economic Theory by M.L JHINGAN

5. Micro Economic Theory by M.L JHINGAN
6. Introductory Economics by STANLAKE'S

**GEOGRAPHY:**

1. Landforms in Africa by COLIN BUCKLE.
2. Principles of Physical Geography by MONKHOUSE.
3. Geography. Integrated Approach by WAUGH.
4. Practical Geography for Africa by J.M. PRITCHARD.
5. AFRICA by J.M. PRITCHARD.
6. Tropical Lands by MICHAEL SENIOR.
7. Human and Economic geography by MORGAN.

**MATHEMATICS:**

1. Pure Mathematics by K.J. BACKHOUSE (1&2)
2. Advanced level Math's Vol. 1 by L.K. SHAYO.
3. Modern ABC.
4. Advanced Level Pure Mathematics, fourth Edition by C.J TRANTA
5. Advanced Mathematics For class XI&XII by CHAND
6. Engineering Mathematics by JOHN BIRD

**PHYSICS:**

1. Principle of physics XI by Chand
2. Principle of physics XII by Chand
3. Understanding Physics by Jim Breclhaupt
4. Objective of Physics by Chand
5. Advance Physics by Roger Munchester
6. Physics by Tom Duncan
7. Calculation for A Level physics
8. Physics ABBOT

**CHEMISTRY:**

1. Conceptual chemistry xi xii –by S.chand
2. Inorganic chemistry –By Ngaiza
3. Advanced inorganic Chemistry vol.1 & 2 –By shand
4. Organic chemistry part A by Tanzania publishing House
5. Organic chemistry part B Tanzania publishing House
6. Physical chemistry by Schand
7. Advanced chemistry –By Cambridge low price Edition Philip Mathew.

8. A level chemistry- 4th Edition EN Ramsiden
9. Practical chemistry –By Mungu.

**HISTORY BOOKS**

1. Major events in African History 1&2

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Basic Applied Mathematics for Form five and six By Sillem

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

*Arusha Girls High School,*
*P.O.Box. 16034,*
*ARUSHA*
*Date .______________*

*Ref. AGHS / F.V 2024/2025*

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

Ref. No:

Medical Officer                                        Date: -------------------------

------------------------------------------

------------------------------------------

------------------------------------------

STUDENT’S NAME___________________________________________

COMBINATION______________________________________________

Please examine the named above for fitness for admission as a student of this school.

**PLEASE BRING TO SCHOOL THE DIAGNOSIS FORM**

Thank you.

--------------------------

M.M.KINYAU

HEADMISTRESS

MOBILE NO: 0784258018

**PART B:**

MEDICAL CERTIFICATE

(*To be completed by a Medical Officer*)

I have examined the above named student and consider that she is fit/not fit for studies:

Explanation if any -----------------------------------------------------------------------------------------

-------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Date --------------------------------------------------- Signature ---------------------------------